## TAMKO KUHUSU HALI YA DEMOKRASIA, HAKI YA KUJUMUIKA NA KUJIUNGA NA VYAMA VYA SIASA NCHINI TANZANIA

### Utangulizi

Sisi Asasi za Kiraia chini ya Jukwaa la Wakurugenzi wa AZAKI nchini na tulio tia saini tamko hili, wote kwa pamoja tumeguswa na mwenendo wa demokrasia, haki ya kujumuika na uhuru wa kujiunga na vyama nchini. Tofauti na matarajio yetu na watanzania kwa ujumla, siku za hivi karibuni tumeshuhudia namna ambavyo matukio mbalimbali yamekua yakiashiria ukiukwaji wa haki za kidemokrasia, haki ya uhuru wa kukusanyika na kujiunga na vyama vya saisa. Kama watanzania wenye jukumu kikatiba kulinda mshikamano, umoja, haki na amani ya nchi tumeona ni vyema kuzungumza na kuwashauri viongozi wetu wa kisiasa na wa kiserikali kupitia tamko hili.

Katika hali hiyo, tumeshuhudia ukiukwaji wa haki hizo zinazolindwa kisheria na Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, sheria nyingine za nchi,mikataba ya kikanda na ya kimataifa ambayo imetiwa saini na serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa sehemu ya sheria za nchi. Kwa kuwa asasi za kiraia miaka yote tumekuwa wakosoaji, washauri na wasaidizi wakubwa wa mambo mengi ya kitaifa , tumeona ni busara na vyema zaidi tukachukua nafasi hii kulishauri taifa nini kifanyike ili kuhakikisha ukikwaji wa haki hizi tajwa haziwezi kuwa sababu ya kupelekea kupoteza amani na umoja wa kitaifa.

### Matakwa ya Sheria Kuhusu Demokrasia, Uhuru wa Kujumuika na Kujiunga na Vyama

Ikumbukwe kuwa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayopaswa kuzingatia misingi ya kidemokrasia na kuheshimu haki za msingi za uhuru wa kujumuika na kujiunga na vyama. Msingi wa hili ni Ibara ya 3 ya Katiba ya

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kadhaa. Ibara hii inasema kama ifuatavyo:

*3.-(1) Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa, yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa.*

*(2) Mambo yote yahusuyo uandikishaji na uendeshaji wa vyama vya siasa nchini yatasimamiwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na ya sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo.*

Pia katika Ibara ya 20.-(1), Katiba inaeleza kuwa kila mtu anastahili kuwa huru, bila ya kuathiri sheria za nchi, kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika na kushirikiana na watu wengine, kutoa mawazo hadharani, na hasa zaidi kuanzisha au kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo.

Si hivyo tu, Tanzania imesaini na kuridhia mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa inayotambua haki za binadamu ikiwa ni pamoja na uhuru wa kujumuika na kutoa maoni. Baadhi ya mikataba hiyo ni Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, Mkataba Unaoanzisha Afrika Mashariki, 1999 na mikataba mbalimbali ya kimataifa.

Lengo kubwa la tamko hili; kwanza ni sisi kama raia wa Tanzania kutimiza majukumu yetu na wajibu wetu kikatiba ya kuikosoa, kuishauri na kuisaidia serikali yetu iliyopo madarakani kwa ridhaa yetu wenyewe pale tunapoona kuna mambo hayaendi sawa kwa namna moja au nyingine. Asasi za kiraia mara zote tumekuwa ni wadau wazuri wa maendeleo tusiofungamana na upande wowote wa itikadi yoyote ya kisiasa au ya kidini. Tumekuwa tukiisaidia serikali kutoa ajira nchini, kutoa huduma za jamii vijijini, kutoa msaada wa kisheria, kutoa elimu ya uraia, kulinda katiba, haki za binadamu pamoja na mambo mengine mengi. Hivyo basi, tunatanguliza kusema chochote tunachosema katika tamko hili kimelenga katika kujenga Taifa letu kwa kulinda upendo, mshikamano, haki, usawa na amani ya nchi.

**Hali ya Demokrasia, Uhuru wa Kujumuika na Kujiunga na Vyama**

Katika kipindi cha miaka zaidi ya miwili sasa tumeshuhudia haki za demokrasia, uhuru wa kujumuika na kujiunga na vyama zikizidi kuzorota kila kukicha. Kwetu sisi hali hii tunaitafsiri kama ni mwazo wa kubomoa umoja wa kitaifa na kupoteza amani ya nchi. Ipo mifano kadhaa inayo akisi hali duni ya sasa ya demokrasia nchini:

a) Kutungwa kwa sheria kandamizi ya vyama vya siasa nchini(Maboresho ya 2019), ambayo AZAKI toka mwanzo tulipinga baada ya kuichambua na kuona inakiuka katiba na haki za kisiasa kwa kiwango kikubwa. Sheria hii imekuja kumpa mamlaka makubwa Msajili wa Vyama vya siasa na kumfanya awe ni nyapara wa vyama vya siasa badala ya kuwa mlezi. Kwa sheria hii Msajili anaweza futa chama chochote wakati wowote, huku yeye akilindwa na sheria kwa maamuzi atakayoyatoa.

b) Mwenendo wa muda mrefu wa Msajili wa vyama vya siasa kuonekana kuchukua upande katika mgogoro wa ndani wa chama cha Wananchi - CUF. Msajili kama mlezi wa vyama anapaswa kutokuwa sehemu ya migogoro ya ndani ya vyama.

c) Barua ya Msajili wa Vyama vya Siasa yenye kumbukumbu HA.322/362/2D/98 ya nia ya Msajili wa Vyama vya Siasa kufuta usajili wa kudumu wa chama cha ACT Wazalendo imeleta mkanganyiko miongoni mwa Tanzania. Kwa nchi yetu ambayo ni ya Kidemokrasia inayofuata misingi ya haki na uwazi tusingetegemea Msajili wa Vyama vya Siasa akitoa onyo kali la namna ile kwa tuhuma ambazo hazijathibitika badala yake angetafuta namna nzuri ya kuwaita na kusuluhisha kabla ya kufikiria kuchukua hatua za awali kama mlezi wa vyama vya saisa. Barua hii ilitolewaa mapema na kubeba shutuma nyingi ambazo zingeweza kujadiliwa kati ya chama husika na ofisi ya msajili.

d) Mikutano ya ndani ya vyama vya upinzani imekuwa ikivamiwa na kuzuiliwa kufanyika. Kwa mfano ni juzi tu tumeona namna ambavyo polisi walivamia na kuzuia mkutano wa ndani wa wanachama wa ACT Wazalendo bila kujali kuwa ni haki ya vyama vya siasa kufanya mikutano.

e) Viongozi wa vyama vya siasa kuzuiwa kufanya mikutano ya kisiasa na wabunge na madiwani kuzuiwa kufanya mikutano ya kisiasa hasa ile ya hadhara katika maeneo yaliyo nje ya majimbo yao.

f) Wabunge kadhaa, wanachama wa upinzani waliokuwa wakifanya mikutano kukamatwa na wengine kufunguliwa mashtaka. Kuongeza kwa hali ya kamata kamata ya viongozi na wafuasi wa vyama vya upinzani nchini wakati mwingine bila sababu za msingi ni jambo hatari kwa mustakabali wa Taifa.

g) Vyombo vya usalama hasa Jeshi la Polisi vilivyopaswa kuwa sehemu ya ulinzi na usimamizi wa usalma wakati wa shughuli za kisiasa nchini

vimeonakana kuwa sehemu ya kukandamiza siasa za vyama vingi nchini kwa kuonekana mara nyingi wakiingilia shughuli za wapinzani chini.

h) Viongozi wa Dini, Bunge la Tanzania, AZAKI, Baraza la Vyama Vyama vya siasa nchini, Wanazuoni, Kituo cha Demokrasia nchini kuendelea kufumbia macho mwenendo wa demokrasia nchini ni tishio jingine kwa amani na umoja wa Kitaifa.

e) Maandamano ya amani kuzuiliwa kwa watu wengine kutokana na mirengo yao ya kisiasa au kijamii huku wengine wakionekana wazi wazi kufanya mikutano na maandamano. Hali hii inawagawa watanzania na kufanya wengine wawe na haki zaidi ya wengine. Hofu yetu ni kwamba hali hii ikiendelea tutalijenga Taifa lenye kundi kubwa la watu wanaohisi wametengwa na kubaguliwa katika taifa letu.

**Wito na Ushauri Wetu kwa Serikali, Wanasiasa na Taifa kwa Ujumla**

i. Msajili wa Vyama vya Siasa aache kuvitisha na kuingilia migogoro ya ndani ya vyama vya siasa na badala yake aongozwe zaidi na hekima katika kusimamia misingi ya demokrasia na haki za wananchi wote kujiunga katika vyama wanavyovitaka bila kuwekewa vikwazo visivyotambulika na sheria za nchi yetu.

ii. Viongozi waheshimu sheria za nchi na katiba kwa kuacha kuzia mikutano ya siasa ya ndani na nje.

iii. Vyombo vya usalama zihakikishe mikutano ya ndani na nje ya vyama vya siasa vinalindwa badala ya kupigwa marufuku na kuvurugwa.

iv. Serikali ihakikishe uhuru wa kujumuika, ikiwa ni pamoja na uhuru wa kufanya maandamano ya amani unaheshimiwa na kulindwa na vyombo vya usalama kama sheria za nchi zinavyoelekeza.

v. Tunatoa wito kwa serikali kuheshimu sheria za nchi na mikataba ya kikanda na kimataifa ambazo imeridhia kuifuata na kuitii ili kujiepusha na uvunjifu usiokuwa wa lazima unaoweza kutuingiza kwenye migogoro ya kidplomasia na juimuiya ya kimataifa.

vi. Tunawasihi wanasiasa walioko madarakani na vyama vya siasa vya upinzani waendeshe siasa kwa kuzingatia sheria za nchi na wahakikishe shughuli zao za kisiasa haziwi sehemu ya kuligawa Taifa kisiasa, kidini ama kikanda ili kuendeleza amani na umoja wa kitaifa.

vii. Tunawashauri watanzania wote wakiwemo viongozi wa dini, wanahabari, wanazuoni na makundi mengine yote, tujitokeze mara kwa mara kukosoa na kuishauri serikali pamoja na wanasiasa wa Taifa hili pale tunapoona kuna viashiria vya kupoteza amani yetu. Hii ni kwa sababu madhara yatakayotokana na kuvurugika kwa amani ya nchi yatamgusa kila mmoja hata yule anayefumbia macho baadhi ya vichocheo vya uvunjifu wa amani yetu.

viii. Tunamshauri Mheshimwa Rais wetu, John Pombe Magufuli aone umuhimu wa kukutana na vyama vya upinzani nchini ili kukaa katika meza ya mazungumzo kuhusu malalamiko yao ya muda mrefu sasa.

ix. Tunamshauri Msajili wa Vyama vya siasa kutumia vyombo mbali kama Baraza la Vyama vya Siasa, Kituo cha Demokrasia na viongozi wa dini kutatua changamoto anazoiona katika uendeshaji wa vyama vya siasa chini badala ya kuamua kila jambo bila kushirikisha wadau.

x. Msajili wa vyama vya siasa tunamshauri badala ya kufikiria kuifuta ACT Wazalendo baada ya siku 14 aunde kamati huru itakayojumuisha makundi mengine huru wakiwemo wana AZAKI kuchambua ukweli wa tuhuma zilizokwenda kwa ACT Wazalendo ili kutenda haki kwa pande zote. Lengo iwe ni kujenga na si kujenga chuki na uhasama zaidi.

xi. Kwa kuwa lengo letu ni kujenga na si kubomoa, na pia kwakuwa AZAKI ni wadau wakubwa wa maendeleo, kama itampendeza Mhe Rais tunaomba kuwa na mkutano wa pamoja na yeye ili tuweze kushauriana naye mambo mengi ya kitaifa ikiwemo hili la demokrasia na uhuru wa raia na vyama vyao. Tunaamini demokrasia na siasa ndio msingi na ustawi wa taifa lolote nchini hivyo hatuna njia ya kukwepa kuzungumzia.

xii. Vifungu vyote vya sheria mpya ya vyama vya siasa vibadilishwe ili kutoa uwanja sawa na huru wa kufanya siasa nchini. Endapo itashindikana hivyo tunashauri AZAKI, Watetezi wa haki za binadamu au vyama vya siasa viende mahakamani kuiomba mahakama itengue vipengele vyote kandamizi. Wakati huo huo tunashauri mifumo yetu ya haki hapa nchini kuzingatia sana haki za binadamu wanapokuwa wanatoa maamuzi yao katika mambo mbali yenye maslahi kwa Taifa.

Hatimaye tunaamini kabisa viongozi wetu watasikia na kufanyia kazi ushauri wetu huu kwa lengo la kulinda umoja, mshikamano na amani ya Taifa. Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika.

**Imetolewa leo tarehe 1 Aprili, 2019**

**Na**

1. Tanzania Human Rights Defenders Coalition (THRDC)
2. Civic and Legal Aid Organization (CiLAO)
3. Door of Hope to Women and Youth Tanzania (DHWYT)
4. New Age Foundation
5. Tanzania Peace, Legal Aid & Justice center (PLAJC)
6. YAAPA
7. Sauti ya wanawake Ukerewe
8. TUPACE
9. ARUWE
10. OJADACT
11. Sauti ya Haki Tanzania
12. Initiative for Good Governance and Transparency in Tanzania(IGT)
13. Child Watch
14. Zanzibar Network for Good Governance (ZNGG)
15. MIDECAC
16. Tanzania Tobacco Control Forum (TTCF)
17. CAGBV
18. MACSNET Manyara
19. VOYOHEDE-Mtwara.
20. Sadeline Health Care Trust
21. RUWODI
22. Tanzania Widows Association (TAWIA)
23. Faidika wote pamoja-FAWOPA Tanzania
24. Legal and Human Rights Centre (LHRC)
25. Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA)
26. CEDO(Christian Education Development Organization)
27. Actions for Democracy and Local Governance (ADLG)
28. Pemba Environmental and Malaria Control (PEMCO)
29. Jumuiya ya Maendeleo ya Elimu Pemba (JUMAEWAPE)
30. Tusishindwe Development Organaization (TUDOPE)
31. NCDE Nguvumali

32. Jamii Forums
33. Zanzibar Development Journalists Association (WAHAMAZA)
34. The Zanzibar Fighting Against Youth Challenges Organization (ZAFAYCO)
35. COSITA
36. Save the Mother and Children of Central Tanzania (SMCCT)
37. Jumuiya ya kuendeleza Ufugaji nyuki na Uhifadhi wa Mazingira (JUKUNUM)
38. Resources Advocacy Initiative
39. SAHRiNGON Tanzania Chapter
40. Mtwara NGO's Network (MTWANGONET)
41. Rondo Women's Development Organization (ROWODO)
42. Magata Primary Cooperative Society
43. Pamoja Daima
44. The Popular Inspiring and Relief Organisation (PIRO)
45. Dignity Kwanza -Community Solutions
46. Hakimadini
47. Pingos Forum
48. Tanzania women empowerment in action, (TAWEA) Kigoma
49. Open Mind Tanzania
50. Jumuiya ya kulinda na kutetea haki za wanawake na watoto (JUKUWAM)
51. Zanzibar Association for Children Advancement (ZACA)
52. Base for Education Dissemination
53. Tree of Hope
54. Normadic Pastoraliast's Development Organization (NOPADEO)
55. Livelihood of Children and Development Society (LICHIDE)
56. CESOPE
57. Tanzania Land Alliance (TALA)
58. TUPACE
59. Iringa Press Club (IPC)
60. KOK Foundation
61. Humanity Aid for Development Organisation (HADO)
62. Tanga Paralegal Aid Scheme for Women and Children
63. Humanitarian Resource Unit for the Maginalised (HURUMA)
64. Mbeya Hope for Orphans (MBEHO)
65. Kigoma Ujiji NGO's Network (KIUNGONET)